

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA  
MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A**


**687 VITENDO VYA KUJIFUNZA HAIBA NA MICHEZO**

**Muda: Saa 3**

**Alhamisi, 10 Mei 2018 mchana**

**Maelekezo**

1. Karatasi hii ina sehemu A na B zenye jumla ya maswali **kumi na sita (16)**.
2. Jibu maswali yote katika sehemu A na maswali **manne (4)** kutoka katika sehemu B.
3. Sehemu A ina alama **arobaini (40)** na sehemu B ina alama **sitini (60)**.
4. Simu za mkononi na vitu vyote visivyoruhusiwa **havitakiwi** ndani ya chumba cha mtihani.
5. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako ch akujibia.



## SEHEMU A (Alama 40)

Jibu maswali yote katika sehemu hii.

1. Kwa kutumia hoja nne, eleza kwa nini ni muhimu kuandaa azimio la kazi kabla ya muhula kuanza.
2. Eleza mbinu nne ambazo mwalimu wa Elimu ya Awali anaweza kusaidia michezo ya watoto kuwa na nidhamu.
3. Changanua mambo manne ambayo mwalimu wa Elimu ya Awali anatakiwa kuzingatia wakati anapofanya upimaji kwa watoto katika somo la Vitendo vya Kujifunza Haiba na Michezo.
4. Eleza kwa kifupi faida za watoto kushirikiana katika michezo.
5. Eleza umuhimu wa kutumia mbinu shirikishi katika kufundisha watoto wa Elimu ya Awali. Toa hoja nne.
6. Fafanua kwa kifupi michezo mitano inayokuza na kuimarisha ushirikiano kwa watoto wa Elimu ya Awali
7. Ainisha wahusika wanne na kwa kila mmoja eleza jinsi anavyoweza kuendeleza na kuwajengea watoto tabia njema.
8. Ainisha zana nne zinazoweza kutumika kufundisha watoto kuelewa dhana ya nidhamu katika michezo.
9. Kwa kifupi fafanua michezo minne inayokuza na kuimarisha ushirikiano kwa watoto wa Elimu ya Awali.
10. Bainisha mbinu nne zitakazowasaidia watoto wa Elimu ya Awali kujifunza nidhamu katika michezo.

## SEHEMU B (Alama 60)

jibu maswali manne (4) kutoka katika sehemu hii.

11. Kwa kutoa hoja tano, elezea njia anazoweza kutumia mwalimu katika kupata zana za kufundishia na kujifunzia.
12. Fafanua kwa kina mambo matano yanayosaidia kuleta hamasa katika michezo kwa watoto.

13. Kuna umuhimu wa kuwafundisha watoto wa Elimu ya Awali dhana ya nidhamu katika michezo. Tetea usemi huu kwa hoja tano.
14. Kumfundisha mtoto wa Elimu ya Awali Vitendo vya Haiba na Michezo ni kupoteza muda. Jadili ukitoa hoja tano.
15. Kwa hoja tano, eleza jinsi mazingira yanavyoweza kukuza au kudumaza ujifunzaji na ufundishaji wa Vitendo vya Haiba na Michezo.
16. Eleza njia tano ambazo mwalimu anatakiwa kutumia ili wanafunzi wote katika darasa jumuishi waweze kujifunza vizuri.